**HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI**
**SHULE YA SEKONDARI NEEMA S.L.P 1732 MOSHI**

Kumb Na NSS/ADM/F1/2020/VOL 1/15 Tarehe.........................

MZAZI/MLEZI WA ....................................
YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NEEMA MWAKA 2021
Ninayo furaha ya kukujulisha kuwa mwanao aliyetajwa hapo juu amechaguliwa kujiunga na Shule hii kwa kidato cha kwanza Mwaka 2021.Shule ya sekondari **NEEMA** ipo katika kijiji cha **MAMBA** kata ya **MACHAME UROKI**. Mwanao ni miongoni mwa wanafunzi wachache waliobahatika kupata nafasi hii, hivyo anatakiwa kuonyesha juhudi na bidii katika masomo ya Sekondari kwa kipindi chote awapo Shuleni

Aidha namkaribisha sana ............................................ kujiunga nasi na ninaamini kwamba ataendelea kuonyesha moyo wa kizalendo na bidii katika masomo.
Muhula wa kwanza wa masomo unaanza rasmi tarehe **11.01.2021** saa 1:00 asubuhi, Ni sharti kwamba mwanao ni lazima aripoti siku na tarehe tajwa hapo juu bila kukosa.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:

1. SARE YA SHULE WAVULANA
   - i) Suruali mbili (2) ndefu rangi ya Kijivu ambazo hazibani upana wa chini usizidi inchi 16-18
   - ii) Mashati mawili (2) meupe ya mikono mifupi
   - iii) Tai fupi rangi ya kijivu
   - iv) Viatu jozi mbili rangi nyeusi vya kufunga kamba vinavyoweza kupigwa kiwi.(visigino vifupi na visiwe vya wazi)
   - v) Soksi jozi mbili (2) rangi nyeusi
   - vi) Sweta mbili rangi ya kijivu.
   - Vii)Mkanda wa suruali mweusi wa ngozi usio na madoido
   - Viii)Mwanafunzi atakaevaa modo ataadhibiwa na suruali itakatwa na atarudishwa nyumbani kushona nyingine
   - ix)Huruhusiwi kunyoa kipara wala staili mfano kiduku,panki n.k

   SARE YA WASICHANA
   - i) Sketi mbili (2) ndefu rangi ya Kijivu za marinda box zinazovuka magoti
   - ii) Blauzi mbili (2) nyeupe za mikono mifupi
   - iii) Skafu fupi rangi ya kijivu
   - iv)Viatu jozi mbili rangi nyeusi vya kufunga kamba vinavyoweza kupigwa kiwi. (visigino vifupi na visiwe viatu vya wazi.)
   - v) Soksi za nyeupe jozi mbili (2)
   - vi) Sweta mbili rangi ya kijivu.
   - Vii)Huruhusiwi kusuka nywele wala kunyoa kipara au staili mfano kiduku,panki n.k

**NB. (i) Rangi ya hijabu ifanane na rangi ya shati (iwe nyeupe)**
**(ii)** Sample ya kitambaa cha sketi na suruali utapewa shuleni

**2. VIFAA VYA MICHEZO KWA WOTE**

i) Raba jozi moja / viatu vya michezo.
ii) Bukta nyeusi Kwa wavulana.
iii) Soksi jozi moja nzito dark blue.
iv) Track suti za michezo rangi ya Blue.Kwa wasichana.

**3. VIFAA VYA TAALUMA:**

i) Madaftari makubwa 09 (Counter book Q2 au Q3)
ii) Mkebe wa vifaa vya Hisabati (Mathematical set 1)
iii) Mathematical table (Four figure). Hiki ni kitabu cha Hisabati kila mmoja awe nacho.
iv) Kalamu za wino, Penseli, Kifutio na Rula ndefu ya sentimita 30.
v) Mzazi anashauriwa kumnunulia mwanae vitabu mbalimbali vya masomo ya Sekondari kwa ajili ya kujisomea nyumbani
vi) Begi la kubebea Daftari zake na sio mfuko wa malboro au sport begi, wala usiwe na maandishi au picha picha.
vii) English Dictionary ( Oxford English Dictionary)
viii) Rimu moja (karatasi kwa ajili ya mazoezi na mitihani)

**4. VIFAA VYA CHAKULA**

Sahani na kikombe vya mfupa au alluminium na kijiko
Wazazi/Walezi wawasiliane na Kamati ya Chakula inayoongozwa na ndugu Badi Lema kwa ajili ya masuala yote ya chakula cha watoto wao wawapo Shuleni.Namba ya simu ya M/kiti wa chakula 0754469841/0755063922

**5.MAZINGIRA**

Mwanafunzi aje na fagio la chelewa ,ndoo moja na jembe moja kwa ajili ya usafi wa mazingira ya shule.

**MUHIMU**

Nasisitiza kuwa mahitaji yote yaliyoorodheshwa ni ya lazima na yakamilishwe ili mwanao aweze kupokelewa Shuleni. Penye tatizo au kutokuelewa maagizo haya fika Shuleni kwa msaada zaidi au maelekezo.

**SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII:**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Raisi TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu. Mwanafunzi anatakiwa kuzingatia yafuatayo:-

a) Heshima kwa viongozi, wazazi/walezi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya Shule kulingana na ratiba ya Shule ni lazima
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparation)
d) Kuwahi katika kila Shughuli ndani na nje ya Shule atakazopewa
e) Kufahamu mipaka ya Shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani au nje ya /mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi katika Shule hii
f) Kutunza usafi wa mwili, Mavazi na Mazingira ya Shule
g) Kuvaa sare ya Shule wakati wote anapotakiwa
h) Kuzingatia ratiba nzima ya Shule wakati wote
i) Kutunza mali za umma

**Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa Shule au kusimamishwa shule:-**

a) Wizi, uasherati, Ushoga na ubakaji
b) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi na kadhalika.
c) Kupiga au kupigana
d) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
e) Kudharau Bendera ya Taifa na Wimbo wa Taifa
f) Kuoa au kuolewa, kuwa mjamzito/kupata mimba au kutoa mimba
g) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki katika kuvuruga amani na usalama wa Shule au Watu.
h) Kukataa adhabu kwa makusudi
i) Kuwa na simu ya Mkononi

**ELIMU NI UFUNGUO WA MAISHA**

**KARIBU SANA NEEMA SEKONDARI**

**A.J.Ringo**
**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI NEEMA
S.L.P. 1732 - MOSHI

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI**

**SHULE YA SEKONDARI NEEMA**

**S.L.P 1732 MOSHI**

## HATI YA UTII WA SHERIA

**A: MWANAFUNZI**

JINA LA MWANAFUNZI ..................................................................................

TAREHE YA KUZALIWA ..................................................................................

JINA MZAZI/MLEZI ..................................................................................

UHUSIANO WA MLEZI (BABA, MJOMBA, KAKA N.K) ........................................

KAZI YA MZAZI/MLEZI ..................................................................................

Mimi ................................................................ Nikiwa mwanafunzi wa shule hii, nakubali kuwa, umma wa nchi hii ya Tanzania ndiyo uliyonipa nafasi hii maalumu ya masomo, ili nimalizapo niweze kuitumikia nchi katika kuleta maendeleo. Hivyo basi ninaahidi kwamba, nitajibidisha hapa shuleni na pia nimalizapo shule. Ili kutimiza shabaha hiyo na ninakubali na kuahidi kwa hiari yangu mwenyewe kuwa nitatii sheria za shule na amri nitakazopewa na uongozi wa shule (walimu na serikali ya wanafunzi). Nikiwa na malalamiko au maoni nitayafikisha kwa uongozi wa shule kufuatana na utaratibu uliowekwa bila kuogopa chochote.

Tarehe ................................................................ Saini ....................................

**B: MZAZI/MLEZI**

Mimi Bwana/Bibi ........................................... Mzazi/Mlezi wa ..............................
Nimesoma kwa makini sheria za shule kama zilivyoandikwa katika maagizo kwa wazazi na nazikubali sheria hizo na nitashirikiana na shule kuona kuwa mwanangu anazingatia kwa makini kwa manufaa ya Umma.

*Tarehe* .................................. *Saini* .................... *Namba ya simu* ...........................

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI**
**SHULE YA SEKONDARI NEEMA**
**S.L.P 1732 MOSHI**

**TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI**

(Taarifa hii ijazwe na wanafunzi wote wa kidato cha kwanza na wanafunzi wanaohamia katika shule hii)

JINA LA KWANZA .................................................................................................

TAREHE YA KUZALIWA ........................................................................................

KABILA ...................................................................... URAIA .....................................

DINI ........................................................................... DHEHEBU ..............................

JINA LA BABA ................................................................................ HAI/AMEFARIKI

JINA LA MAMA ............................................................................... HAI/AMEFARIKI

JINA KAMILI LA MLEZI (KAMA HANA WAZAZI) ......................................................

UHUSIANO NA MLEZI ..........................................................................................

KAZI YA BABA/MAMA/MLEZI ..................................................................................

NAMBA YA SIMU YA MZAZI/MLEZI.........................................................................

ANUANI YA NYUMBANI ........................................................................................

NAMBA YA SIMU YA MZAZI/MLEZI .......................................................................

ULEMAVU WOWOTE WA VIUNGO/AKILI ....................................................................

***NB: Ambatanisha cheti cha kuzaliwa***

**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**HAI DISTRICT COUNCIL**
**NEEMA SECONDARY SCHOOL**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

To be completed by a Medical Officer in respect of all Form One Students and Students who join the school.

**PART A:**
**TO THE MEDICAL OFFICER**

....................................................

Student's Full Name: ________________________________ Sex ________ Age _____

Please examine the above named person as is to be admitted to secondary school education

Signature ....................................... Designation: HEADMASTER

Name of Head of School: KIULA, P. E. Official Stamp ....................................

PART B: TO BE COMPLETED BY A MEDICAL OFFICER

Blood count (red and white) ..............................................................................

Eye test ............................................ T.B. Test ...............................................

Chest ............................................... Ears ......................................................

Abdomen .......................................... Spleen ...................................................

Pregnancy (Girls only) ......................................................................................

Any other test ....................................................................................................

**ADDITIONAL INFORMATION** (e.g. Physical Defect or Impairments)

.....................................................................................................................

.....................................................................................................................

Infectious, Chronic or Family diseases etc. ........................................................

.....................................................................................................................

Please certify that the above is fit to be admitted/taken care in Secondary School.

Kind of care .....................................................................................................

**PART C: MEDICAL OFFICER'S CERTIFICATE**

I have examined the above named person and consider that he/she is not physically fit for joining Secondary Education.

Doctor's name ................................................ Signature ................................

Station ........................................................ Date .........................................

....................................................

***Official Stamp***